**HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO MHESHIMIWA PROF. MAKAME M. MBARAWA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika mkutano huu ambao ni wa kwanza wa bajeti tangu kuingia madarakani kwa Serikali ya Awamu ya Tano.

3. ***Mheshimiwa Spika***, naomba nichukue fursa hii kwa heshima kubwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa na Watanzania kuiongoza nchi yetu katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2015. Kwa kipindi kifupi alichokaa madarakani, Watanzania kwa ujumla wetu tumefarijika na uongozi wake mahiri ambao unaonesha nia ya dhati ya kuiwezesha nchi yetu kupiga hatua kubwa kimaendeleo kwa kasi inayotakiwa. Ninaungana na Watanzania kumuombea afya njema ili aweze kuikamilisha kazi hii kubwa aliyoianza.

4. ***Mheshimiwa Spika***, kwa dhati kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kunipa dhamana ya kuongoza Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Napenda kumuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania wenzangu kuwa sitawaangusha.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ninampongeza pia Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb.), kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, napenda kukupongeza wewe binafsi Mhe. Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuchagu1iwa kuliongoza Bunge letu Tukufu. Napenda pia kuwapongeza Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa kuteuliwa pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwao kuwawakilisha wananchi katika Bunge hili.

**B. MAJUKUMU YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

6. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano iliundwa mwezi Novemba, 2015 baada ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani. Wizara hii inajumuisha sekta kuu tatu ambazo ni Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Nitaeleza kwa kifupi majukumu ya kila sekta.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Ujenzi imekabidhiwa majukumu ya kusimamia Sera ya Taifa ya Ujenzi (2003) na utekelezaji wake pamoja na Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani (2009) na utekelezaji wake; ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko na kusimamia Taasisi zilizo chini ya Sekta.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Sekta ya Uchukuzi, majukumu ni pamoja na kusimamia Sera ya Taifa ya Uchukuzi (2003) na utekelezaji wake; ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi; usafiri na usafirishaji kwa njia ya reli, anga na viwanja vya ndege; utoaji wa leseni za usafirishaji; usalama katika usafirishaji na hali ya hewa, kusimamia Taasisi zilizo chini ya Sekta.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano ina majukumu ya kusimamia Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003; Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya mwaka 1997; na Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2003. Aidha, Sekta ya Mawasiliano ina dhamana ya kuhakikisha kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) vinachangia katika maendeleo ya nchi yetu, pamoja na usimamizi wa majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mawasiliano.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na Mpango na Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa mtiririko wa kisekta nikianzia na Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na hatimaye Mawasiliano.

## C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA 2015/2016

11. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/2016), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020, Malengo ya MKUKUTA II, Ahadi na Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Serikali na Sera nyinginezo za Kisekta, Kitaifa na Kimataifa.

### C.1 SEKTA YA UJENZI

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

12. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Sekta ya Ujenzi ilitengewa kiasi cha **Shilingi bilioni 40.023** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi Aprili, 2016 **Shilingi bilioni 29.934** zilikuwa zimetolewa na HAZINA.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/2016, Sekta ya Ujenzi ilitengewa **Shilingi bilioni 883.832** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi bilioni 191.619** na **Shilingi bilioni 85.572** zilikuwa fedha za nje. Kwa upande wa fedha za Mfuko wa Barabara zilitengwa **Shilingi bilioni 606.64**.

Hadi Aprili, 2016 fedha zilizotolewa ni **Shilingi trilioni 1.08.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 607.35** ni fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, **Shilingi bilioni 149.502** ni fedha za nje na **Shilingi bilioni 323.952** ni fedha za Mfuko wa Barabara. Sehemu kubwa ya fedha za ndani zilizotolewa imetumika kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa miradi ya barabara.

### Utekelezaji wa Miradi ya Barabara na Madaraja

14. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2016, jumla ya **kilometa 414.3** kati ya **kilometa 523** za barabara kuu zilizopangwa kujengwa kwa kiwango cha lami zimekamilika. Aidha, **kilometa 82.4** kati ya **kilometa 113** za barabara kuu zilizopangwa kukarabatiwa kwa kiwango cha lami zimekamilika. Vilevile, Serikali imeendelea na ujenzi wa madaraja makubwa **11** ambapo madaraja ya Nyerere (Kigamboni) na Lukuledi II yamekamilika.

Kwa upande wa barabara za mikoa, jumla ya **kilometa 52.19** kati ya **kilometa 77** zilizopangwa kujengwa kwa kiwango cha lami zimekamilika na jumla ya **kilometa 676** za barabara za mikoa zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe kati ya **kilometa 1,252** zilizopangwa kufanyiwa ukarabati katika mwaka wa fedha 2015/2016.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa yalihusisha matengenezo ya kawaida *(routine and recurrent maintenance)* **kilometa 31,883**, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi **kilometa 6,096** na matengenezo ya madaraja **3,332**. Hadi kufikia Aprili, 2016, jumla ya **kilometa 5,968.5** na madaraja **772** yalifanyiwa matengenezo katika barabara kuu. Kwa upande wa barabara za mikoa jumla ya **kilometa 12,777** na madaraja **648** yalifanyiwa matengenezo.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam, Wizara inatekeleza mradi wa ujenzi wa Barabara ya Juu (Flyover) ya TAZARA, *Interchange* ya Ubungo na maandalizi ya ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya barabara katika maeneo ya Chang'ombe, Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA, Uhasibu (Kurasini) na Morocco. Kuhusu *Flyover* ya TAZARA*,* mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 15 Oktoba, 2015 na ujenzi ulizinduliwa tarehe 16 Aprili, 2016.

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya juu (Interchange) katika makutano ya Ubungo umekamilika chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia. Zabuni kwa ajili ya ujenzi zilitangazwa tarehe 20 Januari, 2016 na zinatarajiwa kufunguliwa Juni, 2016. Aidha, ujenzi wa *flyovers* za Chang'ombe na Uhasibu utafanyika katika Awamu ya Pili ya Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT II) utakaogharamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa *flyovers* katika makutano ya barabara katika maeneo ya Magomeni, Mwenge, Tabata, KAMATA na Morocco zinaendelea.

17. ***Mheshimiwa Spika***, maelezo zaidi kuhusu utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja katika mwaka wa fedha 2015/2016 yamo katika **ukurasa wa 8 hadi 45** wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**Utekelezaji wa Miradi ya Vivuko**

18. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu miradi ya vivuko, hadi kufikia Aprili, 2016, kazi zilizokamilika zimeelezwa kwa kina kwenye kitabu cha Bajeti kuanzia **ukurasa wa 46 mpaka ukurasa 49.**

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuratibu na kuimarisha shughuli za usalama barabarani, mazingira na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara, katika mwaka 2015/2016 Wizara imekamilisha miradi mbalimbali kama ilivyoelezwa kwenye kitabu cha Bajeti **kuanzia uk 51 mpaka 53**.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kurahisisha biashara na usafirishaji kati ya bandari ya Dar es Salaam na nchi jirani za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali imeamua kupunguza vizuizi barabarani, hivyo magari makubwa yanayosafiri kupitia Ukanda wa Kati (Central Corridor) yanapima uzito katika vituo vitatu tu vya mizani ambavyo ni Vigwaza (Pwani), Njuki (Singida) na Nyakahura (Kagera). Vilevile, magari makubwa yanayosafiri kwenda nchi jirani za Jumuiya ya Ushirikiano wa Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kupitia Ukanda wa Dar es Salaam (Dar es Salaam Corridor) yaani barabara ya Dar es Salaam – Tunduma na Uyole – Kasumulu yanapimwa uzito katika vituo vinne tu vya mizani ambavyo ni Vigwaza (Pwani), Mikumi (Morogoro), Makambako (Njombe) na Mpemba (Songwe).

21. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo kuhusu utendaji wa taasisi zilizo chini ya Sekta ya Ujenzi yameoneshwa kwa kina katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia **ukurasa wa 53 hadi 63**.

## C.2 SEKTA YA UCHUKUZI

22. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 389.437.** Kati ya hizo, **Shilingi bilioni 276.032** ni fedha za Maendeleo na **shilling bilioni 113.404** ni fedha za Matumizi ya Kawaida. Hadi Aprili, 2016, fedha za Miradi ya Maendeleo **Shilingi bilioni 147.043,** sawa na asilimia 53 zilikuwa zimetolewa na fedha za Matumizi ya Kawaida **Shilingi bilioni 63.464** sawa na asilimia 56 zilikuwa zimetolewa.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

### Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Mijini na Uchukuzi kwa Njia ya Barabara

***Mheshimiwa Spika,*** msongamano wa magari katika usafiri kwenye majiji na baadhi ya miji umeendelea kuwa changamoto. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imeiagiza SUMATRA ifanye utafiti kuhusu vyanzo, madhara na namna bora ya kukabiliana na msongamano wa magari katika miji na majiji nchini. Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya utafiti huo katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza ataanza kazi mwaka 2016/2017. SUMATRA imeendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vya usafiri kwa nchi nzima na kutoa elimu ya usalama kwa umma ili kupunguza wimbi la ajali na vifo vitokanavyo na ajali za barabarani.

## USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA RELI

### Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO)

***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uchukuzi kupitia RAHCO imeendelea utekelezaji wa miradi ya uboreshaji wa njia ya reli ya kati na upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa miradi ya reli ya sehemu mbalimbali nchini kwa kiwango cha *standard gauge.* Maelezo yakina yanapatikana kwenye cha kitabu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia **ukurasa wa 69 hadi 75.**

### Kampuni ya Reli Tanzania (TRL)

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Reli (TRL) kwa sasa ina vichwa vya treni 25 ikilinganishwa na vichwa 14 vilivyokuwepo mwaka 2014/2015. Mabehewa ya mizigo yameongezeka kutoka mabehewa 530 kwa mwaka 2014/2015 hadi kufikia 704 mwaka 2015/2016. TRL inaendelea na utaratibu wa kuunda upya vichwa vya treni na hadi Aprili, 2016, jumla ya uundaji wa vichwa vipya vya treni vinne (4) kati ya vinane (8) vya awamu ya pili ilikuwa imekamilika.

**Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**

***Mheshimiwa Spika,*** Serikali za Tanzania na Zambia zimeendelea na juhudi za uboreshaji na uendelezaji wa miundombinu na huduma za reli ya TAZARA kupitia Itifaki ya 15. Miradi iliyotekelezwa na kukamilika kupitia Itifaki hii yameelezwa kwa kina kwenye cha kitabu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia **ukurasa wa 75 hadi 77.**

**USAFIRI NA UCHUKUZI MAJINI**

**Huduma za Uchukuzi katika Maziwa**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, huduma za uchukuzi katika maziwa zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Huduma za Meli katika Maziwa (MSCL) pamoja na sekta binafsi. Katika kipindi hicho, MSCL iliendelea kukabiliwa na tatizo la ubovu wa meli za MV Victoria, MV Liemba, MV Songea na MV Clarias. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa wa meli hizo.

**Huduma za Bandari**

***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, Mamlaka ya bandari ilihudumia jumla ya tani milioni 11.73 za shehena ikilinganishwa na tani milioni 12.28 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014/2015. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, Kitengo cha Makasha (TICTS) kilihudumia makasha 355,730 ikilinganishwa na makasha 344,517 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2014/2015. Maelezo ya kina kuhusu utendaji wa Mamlaka wa Bandari yanapatikana katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia **ukurasa wa 79 hadi 88.**

25. ***Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya kuanza mradi wa ujenzi wa Bandari ya Mbegani, Bagamoyo yanaendelea vizuri chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Vipengele vya Mikataba ya Mradi baina ya Serikali na Wawekezaji vilisainiwa tarehe 16 Oktoba, 2015. Aidha, zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa bandari hii wapatao 2,211 wa vijiji vya Pande na Mlingotini ikiwa ni pamoja na sehemu ya Chuo cha Maendeleo ya Uvuvi cha Mbegani (FETA) lilianza Septemba, 2015.

## USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA ANGA

### Udhibiti wa Usalama wa Usafiri wa Anga

***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) imeendelea kusimamia uboreshaji wa viwanja vya ndege nchini ili viendelee kukidhi matakwa ya viwango vya Kimataifa. Aidha, viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Amani Abedi Karume na Kilimanjaro vilikaguliwa tena na kupewa vyeti vya ubora baada ya kukidhi vigezo vya kimataifa vya viwanja vya ndege vya kuweza kupokea ndege kubwa.

### Huduma za Viwanja vya Ndege

26. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka inaendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la Tatu la Abiria (Terminal III Building) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA). Kwa sasa Mradi huu umekamilika kwa asilimia 65 na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2016. Awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha JNIA itaongeza uwezo wa jengo kuhudumia abiria hadi milioni 6 kwa mwaka. Ujenzi wa awamu ya pili unatarajiwa kukamilika Desemba, 2017.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA), Mwanza, Songwe, Bukoba na maandalizi ya ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege kumi na moja (11) vya Lake Manyara, Musoma, Iringa, Tanga, Songea, Kilwa Masoko, Lindi, Moshi, Njombe, Simiyu na Singida kwa kiwango cha lami yanapatikana katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti **kuanzia ukurasa 95 hadi 100.**

**Huduma za Usafiri wa Ndege**

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2015 hadi Aprili, 2016, ATCL ilitoa huduma ya usafiri wa anga kati ya Dar es Salaam na Mwanza, Mtwara, Kigoma na Moroni, Comoro kwa kutumia ndege yake aina ya Dash 8-Q300 na ndege ya kukodi aina ya CRJ 200. Katika kipindi hicho, ATCL ilisafirisha abiria 32,434 ikilinganishwa na abiria 30,246 waliosafirishwa mwaka 2014/2015.

**HUDUMA ZA HALI YA HEWA**

29. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2015/2016, Mamlaka ilikamilisha kazi ya uboreshaji wa mfumo wa mawasiliano na uchambuzi wa *data* za hali ya hewa katika Kituo Kikuu cha Taifa cha Utabiri pamoja na vituo vilivyo katika viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Zanzibar, Mwanza na Kilimanjaro.

**C.3 SEKTA YA MAWASILIANO**

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

30. ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2015/2016, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa kiasi cha **Shilingi bilioni 43.195** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi Aprili, 2016 **Shilingi bilioni 29.081** zilikuwa zimetolewa na HAZINA.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2015/2016, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa **Shilingi bilioni 15.798** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi Aprili, 2016 fedha zilizotolewa ni **Shilingi bilioni 2.766**. Kati ya fedha hizo**, Shilingi bilioni 2** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 766.062** ni fedha za nje.

**Ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano**

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano imekua kwa kasi kubwa ambapo ukuaji huu unathibitishwa na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano. Mafanikio ya sekta yameelezwa kwa kina kwenye kitabu cha hotuba ya Bajeti kuanzia **uk. 105 mpaka uk 107.**

**Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano ina simamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano- Awamu ya III na IV. Awamu ya III sehemu ya I inajumuisha ujenzi wa kituo mahiri cha kutunzia kumbukumbu (Internet Data Centre) Dar es Salaam, miundombinu ya mtandao wa itifaki (Internet Protocol-Multilayer Label Switching - IP/MPLS Service), na uunganishaji wa Zanzibar katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na utekelezaji wake umekamilika mwezi Aprili 2016.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Awamu ya IV inayohusu ujenzi wa Mikongo ya Mijini (Metro Fibre Ring Networks) na *Missing Links* ya Mkongo wa Taifa imeanza na inatekelezwa kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano (operators) nchini. Jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 80 zitatumika katika mradi huu.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano imekamilisha ujenzi wa mtambo wa *Internet Bandwidth* na ununuzi wa *Internet Bandwidth* yenye ukubwa wa *1.55 Gbps* ambayo tayari imeanza kutumika na hadi hivi sasa zaidi ya taasisi za Serikali 170 zinatumia huduma ya internet kwa bei nafuu.

**Juhudi za Serikali Kufikisha Huduma ya Mawasiliano Vijijini**

36. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano kwa kushirikiana na Kampuni ya VIETTEL (Viettel Joint Stock Company – VIETTEL) ya Vietnam inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya Mawasiliano Vijijini. Hadi Aprili, 2016 kazi zifuatazo zimetekelezwa:

i) Kukamilisha ujenzi wa kilometa 18,000 za Mkongo katika Wilaya zote nchini;
ii) Ujenzi wa miundombinu ya mawasailiano katika vijiji 2,208,
iii) Kuendelea kuunganisha kwenye mkongo Ofisi zote za Wakuu wa Wilaya, Hospitali za Wilaya, Ofisi 65 za Posta na Ofisi zote za Polisi za Wilaya nchini, na
iv) Kuzipatia intaneti shule za sekondari 431 za Wilaya.

**Mpango wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatekeleza mradi wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta ili kuboresha shughuli za kijamii na kiuchumi. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta yanapatikana katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia **ukurasa wa 111 mpaka 112.**

**Mradi wa *Video Conference***

38. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha matumizi ya TEHAMA yanakua hasa katika ofisi za Serikali, Sekta ya Mawasiliano imekamilisha ufungaji na usimikaji wa mitambo ya *Video Conference* ambayo tayari imeanza kutumika kwenye Makao Makuu ya Mikoa 22 ya Tanzania Bara, Ofisi 3 za Serikali kuu na ofisi 5 za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

39. ***Mheshimiwa Spika*, ** utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mawasiliano umeoneshwa kwenye **ukurasa 116 hadi 123** wa Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti.

**D. CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA**

***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa majukumu yake Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo pamoja na mikakati ya kukabiliana nazo zimeoneshwa kwenye **ukurasa 142 hadi 146** wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Wizara.

**E. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

**E.1 SEKTA YA UJENZI**

**Matumizi ya Kawaida**

40. ***Mheshimiwa Spika,*** bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu 98 - Ujenzi) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni **Shilingi bilioni 35.936.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 34.287** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi bilioni 1.649** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya sekta ya Ujenzi na Taasisi zake.

**Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

41. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/2017, sekta ya ujenzi imetengewa jumla ya **Shilingi trilioni 2.176** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo**.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 1.248** ni fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi bilioni 344.838** ni fedha za nje. Aidha, **Shilingi bilioni 582.644** ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara. Mgawanyo huo umeonesha kwenye ***Kiambatisho Na.1*** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti. Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo:

**Miradi ya Vivuko**

42. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya vivuko imetengewa **Shilingi bilioni 15.50** kama ilivyoonesha kwenye ***Kiambatisho Na.1.***

**Miradi ya Nyumba na Majengo ya Serikali**

43. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, jumla ya **Shilingi bilioni 7** zimetengwa kwa ajili ya miradi ya nyumba na majengo ya Serikali kama ilivyooneshwa kwenye **ukurasa wa 148 hadi 151** wa Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti.

**Miradi ya Barabara na Madaraja**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/2017 jumla ya **Shilingi trilioni 1.569** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara kuu zenye urefu wa **kilometa 592** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **14** pamoja na ukarabati wa **kilometa 146.5** kwa kiwango cha lami. Aidha, **Shilingi bilioni 30** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zimetengwa kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami **kwa** barabara za mikoa zenye urefu wa **kilometa 63.8** pamoja na ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa **kilometa 712.40**. Orodha ya miradi ya barabara za mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

45. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya malipo ya Makandarasi na Wahandisi Washauri waliokamilisha miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara na madaraja.

46. ***Mheshimiwa Spika***, miradi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami inayoendelea kutekelezwa iliyotengewa fedha ambayo baadhi yake inatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2016/2017 ni pamoja na barabara za Kyaka – Bugene (km 59.1); Ndono – Urambo (km 52); Tabora – Nyahua (km 85); Dodoma – Babati (km 251.4); Tunduru - Mangaka – Mtambaswala (km 202.5); Tunduru – Matemanga – Kilimasera - Namtumbo (km 193); Sumbawanga - Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 151.6); Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112); KIA – Mererani (km 26); Uyovu – Bwanga - Biharamulo (km 112); Arusha – Moshi – Holili (sehemu ya Sakina – Tengeru: km 14.10 na Arusha *Bypass:* km 42.4); Nyakanazi – Kibondo (km 50); Kidahwe – Kasulu (km 50); Makutano – Natta – Mugumu (km 125); Nansio – Kisorya – Bunda (sehemu ya Bulamba – Kisorya: km 51); Tabora – Sikonge (sehemu ya Tabora – Usesula, km 30); Kikusya – Ipinda – Matema Beach (sehemu ya Tenende – Matema: km 34.6); Kaliua – Kazilambwa (km 56); Igawa - Mbarali - Ubaruku sehemu ya Mbarali - Ubaruku (km 8.9) na Magole –Turiani (km 48.8). Aidha, madaraja makubwa yatakayoendelea kujengwa na kukamilika katika

mwaka wa fedha 2016/2017 ni pamoja na Daraja la Kilombero (Morogoro), Daraja Jipya la Ruvu Chini (Pwani), Daraja la Sibiti (Singida) na Daraja la Kavuu (Katavi).

47. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Serikali itaanza kutekeleza miradi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zifuatazo: Tabora (Usesula) – Ipole – Koga – Mpanda (km 343); Chaya – Nyahua (km 85.5); Uvinza – Malagarasi (km 51.1); Kazilambwa – Chagu (km 40); Urambo – Kaliua (km 28); Mbinga – Mbamba Bay (km 66); Masasi – Newala – Mtwara (sehemu ya Mtwara – Mnivata: km 50); Njombe – Ndulamo – Makete (km 109); barabara ya mchepuo wa Iringa (km 7.3); Mpanda – Mishamo (sehemu ya Mpanda – Usimbili: km 30); Chunya – Makongolosi (km 43); Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa (sehemu ya Itigi – Mkiwa: km 35); Sanya Juu – Kamwanga (sehemu ya Sanya Juu – Elerai: km 32.2); Loliondo – Mto wa Mbu (sehemu ya Wasso (Loliondo) – Sale Junction: km 50); Njombe – Lupembe – Madeke (km 50); Tengeru – Holili (km 108); Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152) na Itoni – Ludewa – Manda (sehemu ya Lusitu – Mawengi: km 50). Madaraja yatakayoanza kujengwa ni pamoja na Daraja la Momba (Rukwa/Songwe), Daraja la Ruhuhu (Ruvuma/Njombe), Daraja la Simiyu (Mwanza) na Daraja la Mara (Mara).

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara itakamilisha upembuzi yakinifu wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 200) sehemu ya Dar es Salaam – Chalinze (km 128) kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha *Expressway*. Aidha, Wizara itaanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Same – Kisiwani – Mkomazi (km 96.7); Arusha - Kibaya-Kongwa (km 430); Tarime – Mugumu (km 86); Nanganga - Ruangwa – Nachingwea (km 100); Uyole – Mbalizi (Songwe Bypass – km 40); Isyonje – Kikondo – Makete (km 96.2); Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River– Lalago - Maswa (km 386); Kibada - Mwasonga - Kimbiji (km 19.2); Kimbiji - Tundwisongani (km 30.5); Tegeta-Bagamoyo (km 43.2); Makofia-Mlandizi (km 36.7); Mbegani-Bagamoyo (km 7.2); Kibondo - Mabamba (km 45); Nyamirembe Port – Katoke (km 50) pamoja na Daraja litakalounganisha Kigongo na Busisi na Daraja la Muhimbili litakalounganisha eneo la Muhimbili na Mkwajuni (Kinondoni).

49. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara imetenga fedha kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Miradi hiyo ni ujenzi wa barabara za Kawawa Roundabout – Msimbazi Valley – Jangwani/Twiga Jct (km 2.7), Tabata Dampo – Kigogo (km 1.6), Kimara – Kilungule – External (km 9.0), Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 14.0), Tegeta – Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi (km 20) sehemu ya Goba – Mbezi Mwisho (km 7), Tangi Bovu – Goba (km 9.0), Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.60) pamoja na *Flyover* ya TAZARA.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zinazotarajiwa kuanza ni ujenzi wa *Interchange* ya Ubungo, maandalizi ya ujenzi wa Daraja jipya la Selander, maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili (BRT II) itakayohusisha barabara za Kilwa, Chang'ombe na ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Chang'ombe na Uhasibu, upanuzi wa daraja la Mlalakuwa na uboreshaji wa mifereji ya maji ya mvua kwenye barabara ya Mwenge – Tegeta (km 12.9). Kazi nyingine ni upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki, ujenzi wa barabara za Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (sehemu ya Kitunda – Moshi Bar, km 3.2), Ardhi – Makongo (sehemu ya Goba – Makongo - km 4.00), Maji Chumvi – Chang'ombe – Barakuda (km 2.5), Mjimwema – Vijibweni, Tungi – Kibada na Kibada – Mjimwema pamoja na kuanza ujenzi wa mizani ya kupima magari karibu na Bandari ya Dar es Salaam. Aidha, Serikali itaanza maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka awamu ya tatu (BRT III) utakaohusisha barabara ya Nyerere (kuanzia Gongo la Mboto hadi katikati ya Jiji (CBD), barabara ya Uhuru, barabara ya Bibi Titi Mohamed na Azikiwe zenye jumla ya kilometa 23.6. Mradi huu unatarajiwa kugharamiwa na Benki ya Dunia.

Maelezo ya kina kuhusu miradi ya barabara na madaraja itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 yameoneshwa katika **ukurasa wa 153 hadi 175** katika Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti.

**Fedha za Mfuko wa Barabara**

51. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/2017, Mfuko wa Barabara unatarajiwa kukusanya jumla ya Shilingi **bilioni 832.349** zitakazotumika kufanya kazi za matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, Sekta ya Ujenzi na Taasisi zake imetengewa Shilingi **bilioni 582.644** na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imetengewa Shilingi **billion 249.704**.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya Shilingi **bilioni 582.644** zilizotengwa kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano , sekta Ujenzi imetengewa Shilingi **bilioni 57.763** kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko. Mchanganuo wa miradi hiyo umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3** cha Kitabu cha Hotuba ya Bajeti. Aidha miradi ya barabara za mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 4** cha Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Barabara umetengewa Shilingi **bilioni 519.87** kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yatahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) **kilometa 22**,**839**, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofi ya **kilometa 4,749** na matengenezo ya madaraja **2,821**. Muhtasari wa mpango wa matengenezo ya barabara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 5** katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

***Mheshimiwa Spika,*** maelezo ya kina kuhusu mpango wa utekelezaji kazi katika taasisi zilizo chini ya Sekta ya Ujenzi katika mwaka wa fedha 2016/2017 yametolewa katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara **ukurasa 176 hadi 187.**

## E.2 SEKTA YA UCHUKUZI

### Matumizi ya Kawaida

54. ***Mheshimiwa Spika,*** bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Sekta ya Uchukuzi (Fungu 68) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni Shilingi **bilioni 91.519.** Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni **52.430** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na Shilingi **bilioni 39.088** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya sekta Uchukuzi na Taasisi zake.

**Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

55. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Sekta ya Uchukuzi imetengewa jumla ya **Shilingi trilion 2.495** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo**.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi trilioni 2.322** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 173.210** ni fedha za nje.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya Uchukuzi imepanga kutekeleza miradi ifuatayo:

(i) Kutandika reli nzito za ratili 80 katika maeneo mbalimbali ya reli ya kati. Kujenga madaraja, makalavati na ujenzi wa stesheni na jengo la kuhifadhia mizigo. Kuboresha eneo la treni la kupakia/kupakua mizigo katika bandari ya DSM, Isaka na Ilala. Pia kununua vipuri vya mtambo wa kuzalisha kokoto wa Tura, ununuzi wa mtambo wa kukagua na kupima njia ya reli na uzalishaji wa mataruma katika karakana ya Pugu. Shilingi bilioni 202.89 zimetengwa;

(ii) Kukamilishi usanifu wa kina, upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa miradi ya reli katika maeneo nchini kwa kiwango cha *standard gauge.* Shilingi bilioni 19.7 zimetengwa;

(iii) Shilingi bilioni 5.0 zimetengwa kwa ajili ya kumwajiri Mshauri wa Uwekezaji atakayesimamia upatikanaji wa fedha pamoja na ujenzi wa reli ya Mtwara – Songea – Mbamba Bay pamoja na matawi ya kwenda Mchuchuma na Liganga (km 1000); na

(iv) Kufanya usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa Reli ya Kati kwa *standard gauge* ambapo Shilingi trilioni 1.0 zimetengwa;

Maelezo ya kina ya miradi hii yanapatikana kwenye cha kitabu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia **ukurasa wa 188 hadi 190.**

57. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Huduma za Meli katika Maziwa (MSCL) imetengewa Shilingi bilioni 50.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa meli moja (1) na ukarabati wa meli za MV Butiama, MV Victoria, na MV Liemba.

***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uchukuzi imetenga Shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kutekeleza miradi wa viwanja vya ndege vya Kigoma, Tabora, Songwe (Mbeya), Mwanza, Mtwara, Sumbawanga na Shinyanga, mkoa wa Geita, Msalato, Bukoba na Julias Nyerere.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Ndege (ATCL) imetengewa shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kununua ndege mpya zisizopungua 3.

Mgawanyo wa fedha za Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Sekta ya Uchukuzi umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 6** cha Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**E.3 SEKTA YA MAWASILIANO**

**Matumizi ya Kawaida**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara kwa upande wa sekta ya Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni Shilingi **bilioni 3.073.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **bilioni 2.161** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na Shilingi **milioni 912.326** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Sekta ya Mawasiliano.

**Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

60. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/2017, Sekta ya Mawasiliano imetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 92.730** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo**.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 5** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 87.73** ni fedha za nje (**Kiambatisho Na 7**).

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Mawasiliano, imepanga kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambao umetilia mkazo katika maeneo mbalimbali ambayo yameorodhesha kwenye kitabu changu cha Bajeti kuanzia **ukurasa 198 hadi ukurasa 200**.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** mpango wa utekelezaji kazi katika Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 umeainishwa katika Kitabu cha Hotuba ya bajeti ya Wizara yangu kuanzia **ukurasa 200 hadi 205.**

**SHUKURANI**

63. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda nitumie fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa. Aidha, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili Tukufu na kwa nafasi ya pekee kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa ushauri wao wenye tija katika kuendeleza Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuzishukuru Nchi Rafiki na Washirika mbalimbali wa Maendeleo walioendelea kushirikiana nasi katika kutekeleza programu na mipango yetu katika kuendeleza Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Nchi hizo na Washirika wa Maendeleo ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), Korea Kusini, Finland, Abu Dhabi Fund, Denmark (DANIDA), Ujerumani (KfW), Marekani (MCC), Uingereza (DFID), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait Fund, OPEC Fund, BADEA, Shirika la Bahari Duniani (IMO), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), UNESCO, Jukwaa la Uchumi Duniani (WEF), Malaysia, Afrika Kusini, Uholanzi, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), TMEA, India, China, Norway, Ubelgiji, Urusi, Sweden, Ufaransa, Singapore, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC na wengine wengi.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano nikianzia na Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani (Mb.), Naibu Waziri; Eng. Joseph M. Nyamhanga, Katibu Mkuu (Ujenzi); Dkt. Leonard M. Chamuriho, Katibu Mkuu (Uchukuzi); Prof. Faustin R. Kamuzora, Katibu Mkuu (Mawasiliano); Eng. Dkt. Maria L. Sasabo, Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano); Wakuu wa Idara na Vitengo; Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kujituma katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru wadau wote wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari ambao wametupa ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru familia yangu hususan mke wangu na watoto kwa kunifariji na kuniombea wakati nikitekeleza majukumu yangu ya kitaifa.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba yangu hii inapatikana katika tovuti za Sekta ya Ujenzi (*www.mow.go.tz*), Sekta ya Uchukuzi (*www.uchukuzi.go.tz*) na Sekta ya Mawasiliano *(www.mst.go.tz*).

**MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILANO KATIKA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

69.***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,895,279,317,500.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,212,141,496,500.00** ni kwa ajili ya Fungu 98 - Ujenzi, **Shilingi 2,587,333,762,000.00** ni kwa ajili ya Fungu 62 - Uchukuzi na **Shilingi 95,804,059,000.00** ni kwa ajili ya Fungu 68 - Mawasiliano. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

**SEKTA YA UJENZI (FUNGU 98)**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi 2,212,141,496,500.00** za Sekta ya Ujenzi (Fungu 98) zinajumuisha **Shilingi 35,936,939,500.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 34,287,474,500.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 1,649,465,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. Shilingi **2,176,204,557,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,248,721,422,000.00** ni fedha za ndani, **Shilingi 582,644,500,000.00** ni za Mfuko wa Barabara na Shilingi **344,838,635,000.00** ni fedha za nje.

**SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU 62)**

71. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi 2,587,333,762,000.00** za Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) zinajumuisha **Shilingi 91,519,632,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 52,430,658,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na Shilingi **39,088,974,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. **Shilingi 2,495,814,130,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,322,603,400,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 173,210,730,000.00** ni fedha za nje.

**SEKTA YA MAWASILIANO (FUNGU 68)**

72. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi 95,804,059,000.00** za Sekta ya Mawasiliano (Fungu 68) zinajumuisha **Shilingi 3,073,949,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 2,161,623,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 912,326,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. **Shilingi 92,730,110,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo, **Shilingi 5,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 87,730,110,000.00** ni fedha za nje.

73. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha Miradi ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 (**Kiambatisho Na. 1 - 7**) ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo. Naomba **viambatisho** hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

74. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.